JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# MKAKATI WA KITAIFA DHIDI YA RUSHWA NA MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA TANZANIA

Ofisi ya Rais,
Ikulu,
Dar es Salaam.

Novemba, 1999

pa wa Serikali, Dar es Salaam – Tanzania

# MKAKATI WA KITAIFA DHIDI YA RUSHWA
# NA
# MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA TANZANIA

YALIYOMO


| SEHEMU | UKURASA |
| --- | --- |
| ORODHA YA YALIYOMO | iii |
| MUHTASARI WA UTENDAJI | 1 |
| 1. UTANGULIZI | 2 |
| 2. SABABU ZA RUSHWA | 3 |
| 3. MALENGO NA KANUNI ZA MKAKATI HUU | 6 |
| 3.1 Malengo | 6 |
| 3.2 Kanuni | 8 |
| 3.2.1 Kinga | 8 |
| 3.2.2 Kutekeleza | 9 |
| 3.2.3 Umma Kutambua na Kushiriki | 9 |
| 3.2.4 Kujenga Taasisi | 10 |
| 4. UTASHI WA KISIASA | 10 |
| 5. MAENEO AULA SABA YA MKAKATI HUU | 11 |
| 5.1 Utawala wa Sheria na Mfumo wa Kisheria | 11 |
| 5.2 Nidhamu na Usimamizi wa Fedha | 11 |
| 5.3 Kununua | 11 |
| 5.4 Kuelimisha Umma, Kutambua na Kujua Haki zao | 11 |
| 5.5 Kurekebisha Utumishi wa Serikali | 11 |
| 5.6 Watoa Habari | 11 |
| 5.7 Vyombo vya Habari | 11 |
| 6. MAMBO MUHIMU KATIKA UTEKELEZAJI WA MKAKATI HUU | 12 |
| 7. MAMBO YANAYOCHOCHEA UENDELEZAJI WA MKAKATI | 13 |
| 7.1 Kuunga mkono Sera | 13 |
| 7.2 Teknolojia Muafaka | 13 |
| 7.3 Uwezo wa Kitaasisi na Kiuongozi | 13 |
| 7.4 Mambo ya Kijamii-Kiuchumi | 13 |

| SEHEMU | UKURASA |
| --- | --- |
| 7.5 Vipengele vya Kijinsia | 13 |
| 7.6 Uwezo wa Kifedha | 13 |
| 8. UTEKELEZAJI WA MKAKATI | 14 |
| 9. UFUATILIAJI NA TATHMINI | 14 |
| 10. MATOKEO | 14 |
| 11. MPANGO | 17 |
| 12. (DAMA) LA MPANGO JUMUIFU NA TONDOTI WA UTEKELEZAJI | 18 |

# MKAKATI DHIDI YA RUSHWA NA MPANGO WA UTENDAJI KWA TANZANIA

## MUHTASARI WA UTENDAJI

Tanzania kama takribani nchi zote za Afrika inakabiliwa na rushwa katika sekta zake za umma na za binafsi ambayo imekuwa ya kiwango cha kutisha. Serikali inaliangalia janga hili kama adui wa kwanza wa umma. Kwa hiyo hatua kadhaa zimechukuliwa kwa kipindi kirefu kushughulikia tatizo hili. Waraka huu wa mkakati ni mfululizo wa jitihada za serikali za kutoa kiunzi cha sera cha kukabiliana na adha hii kwa njia ya mpangilio zaidi na jumlifu.

Kushambulia rushwa kwa uthabiti, ni muhimu kutambua sababu zake za msingi, yaani uchoyo na umaskini. Kuenea kwa mambo haya kunatoa mazingira ya kutendea kazi katika sekta ya umma na ya binafsi yanayopalilia matendo ya rushwa. Hivyo watu wanalazimika "kununua" huduma na upendeleo ili watekelezewe mahitaji yao. Watu wasiokuwa na murua kuchukulia hali hii na kujilimbikizia utajiri wa haramu. Hatimaye uchumi wa nchi unapata athari hasi zisizokuwa na kifani.

Mkakati huu wa Kitaifa dhidi ya rushwa na mpango wa utendaji kisekta vimekusudiwa kuwaelekeza waunda sera, wabunge, maofisa wa sheria na watekelezaji. Mkakati wa kitaifa dhidi ya rushwa una mikabala miwili, yaani, changanuzi na wa kubadili. Mkabala changanuzi unasisitiza marekebisho ya kiasasi. Mkabala wa kubadili unalenga kwenye kuwaelewesha wananchi. Jambo muhimu katika mkakati huu ni kiunzi changamani (changanuzi na amatendo) yaani shirikishi na chenye kutanguliza matendo.

Zaidi ya hayo mkakati umedhamiriwa kuziba pengo baina ya serikali kwa upande mmoja, na raia na sekta binafsi, kwa upande mwingine. Muhimu zaidi, msisitizo unawekwa kwenye kupata uwazi na uwajibikaji katika shughuli za serikali, kwa upande mmoja, na ushirikishwaji wa raia na sekta binafsi.

**Malengo ya mkakati huu yanaungwa mkono na mipango ya sekta ya utendaji kama ilivyowekewa aula katika madama yaliyoambatanishwa. Madama ni vielelezo vya maeneo ya aula ya serikali ambayo yatatakiwa kufuatiliwa mara kwa mara na kufanyiwa tathmini ambayo itatekelezwa na Wizara husika, raia na sekta binafsi.**

# MKAKATI WA KITAIFA DHIDI YA RUSHWA

## 1. UTANGULIZI:

Tangu uchaguzi mkuu wa kwanza wa vyama vingi katika mwaka 1995 moja ya vipaumbele vikuu vya Serikali ya Tanzania kimekuwa ni kuboresha uchumi wa nchi. Ili kufanikisha lengo hili Serikali imeanzisha idadi kadhaa ya marekebisho ya msingi yakiwemo ubinafsishaji, ulegezaji wa masharti ya uchumi na uundaji mpya na uboreshaji wa ufanisi wa utoaji wa huduma za serikali.

Hata hivyo, moja ya vikwazo vikubwa vilivyokwamisha msukumo wa serikali wa kufanikisha kuboresha uchumi imekuwa ni kuenea kwa rushwa iliyostawi katika tabaka zote za jamii. Imesababisha hasara kubwa za uchumi kutokana na upungufu wa mapato yatokanayo na kodi, ushuru na malipo mengine ya kifedha, ukosefu wa mapato kutokana na maliasili na hasara kutokana na matumizi mabaya ya mali za serikali. Kwa jumla hali hii imefanya utawala wa serikali na mahakama visiaminiwe na wananchi. Katika hali kama hii Serikali imeona hapana budi kuchukua hatua kali kupambana na janga hili.

Sera ya Serikali ya mapambano dhidi ya rushwa ni ya kutoivumilia kabisa. Hii inashuhudiwa na jitihada za Serikali za kupambana na rushwa. Katika 1966 serikali iliunda ofisi ya Tume ya Kudumu ya Uchunguzi (ombudsman), ya kwanza ya aina yake katika Afrika. Madhumuni yalikuwa ni kudhibiti matumizi mabaya ya madaraka ya maofisa wa Serikali na mawakala wake. Hii ilifuatiwa na kuanzishwa kwa Kikosi cha Kuzuia Rushwa katika 1975 baada ya bunge kupitisha sheria Na. 16 ya 1971 Sheria ya Kuzuia Rushwa.

Katika mwaka wa 1983 likikabiliana na tatizo la rushwa na dhuluma. bunge lilitunga sheria iitwayo sheria ya kuhujumu uchumi ya 1983. Sheria hii ilidumu kwa muda mfupi na kufutwa haraka na kubadilishwa haraka na sheria ya kudhibiti uchumi na uhalifu (ulioandaliwa) ya mwaka 1984. Sheria hii ilijumuisha makosa yaliyokuwa chini ya sheria ya Kuzuia Rushwa kama makosa ya kiuchumi.

Pia kuna azma ya kisiasa ya kushughulikia rushwa Chama tawala cha CCM kilionyesha katika Ilani yake ya Uchaguzi mwaka 1995 kwamba kinaelewa ukubwa wa tatizo la rushwa nchini. Ilani ilitenga rushwa kuwa ni adui namba moja wa wananchi na kuapa kuwa serikali yake itakoleza vita dhidi yake. Baada ya uchaguzi Serikali ilianzisha hatua kadhaa zilizodhamiriwa kushughulikia tatizo la rushwa.

Bunge lilitunga sheria nyingine (sheria Na. 13 ya 1995) inayojulikana kama (Leadership code of ethics) Miiko ya Uongozi. Sheria hii iliandaliwa kuzuia tabia zisizofaa za viongozi wa umma katika ngazi za juu. Mwishoni mwa mwaka huo. Rais aliteua Tume ya Rais ya uchunguzi Dhidi ya Rushwa (PCIC) inayojulikana zaidi kwa jina la Tume ya Warioba. Tume iliendesha stadi bainishi ya kutaka kujua kwa nini rushwa imekuwa sugu katika jamii ya Tanzania. Huu ulikuwa uthibitisho muhimu wa azma ya Serikali ya awamu ya tatu ya kupambana na baa la rushwa nchini.


Tume iligundua kuwa kuna watu wanaopokea rushwa kama njia ya kujazia kipato chao duni na wale wanaojiingiza katika vitendo vya rushwa kwa sababu ya uchoyo uliokithiri wa kuhodhi utajiri. Kundi la kwanza linawakilisha rushwa uchwara, na la pili linawakilisha kategoria ya rushwa kabambe. Tume, katika ripoti yake, inataja wazi kuwa chanzo kikubwa cha rushwa nchini ni uongozi zembe, ukosefu wa miongozo ya wazi juu ya uwajibikaji wa viongozi, mmomonyoko wa jumla wa maadili ya viongozi. Kuibuka kwa mashindano ya matumizi ya kifahari na mabadiliko katika mazingira ya uchumi huria ambayo yanatoa hisia kuwa mtu anaweza kufanya lolote na asisailiwe na mtu yeyote, haya nayo yalitajwa mahususi.

Kama ilivyoonyeshwa waziwazi, Serikali imedhamiria kuasisi utaratibu wa kushughulikia rushwa katika Tanzania. Hata hivyo haina budi kutajwa kuwa kwa sababu za vikwazo vya uwezo wa kifedha na wa kiasasi serikali imekuwa teuzi sana katika kuchagua njia za kuingilia kati. Zile ambazo zinaweza kutekelezwa haraka kwa gharama ndogo lakini zenye athari ya haja zinaandaliwa kutekelezwa mara moja na nyingine zitapangwa kutekelezwa kipindi cha kati na cha muda mrefu.

## 2. SABABU ZA RUSHWA

Kwa ajili ya mkakati huu ni muhimu kuelewa sababu za msingi za rushwa. Katika jamii yoyote ile kuna mambo mawili yanayosababisha watu wajiingize katika matendo ya rushwa: Uchoyo na umaskini. Kutawaliwa kwa mambo haya huzaa yafuatayo:

**SABABU ZA RUSHWA MTAZAMO CHANGANUZI**




- Kutomudu na uzembe katika kutoa huduma za umma;
- Kasoro za mifumo;
- Viunzi vya Kisheria na Kiutawala/Kisiasa vyenye kutoa mazingira yenye kuendekeza kuwako kwa rushwa;
- Miundo ya Asasi/Mashirika na tabia za uendeshaji zenye kuendekeza rushwa;
- Hali za uchumi zenye kufanya watu watapetape kuishi.

Rushwa inadhihirishwa na uozaji wa asasi. Matumizi mabaya ya ofisi ya serikali kwa shughuli zisizo za kiserikali yanaumiza uchumi, yanazaa umaskini, hudhoofisha uhalali wa serikali, hudhoofisha utawala wa sheria na kuheshimu katiba, hupalilia utendaji duni na husababisha ukosefu wa uwazi na uwajibikaji. Kwa muhtasari, huzuia maendeleo, huharibu utawala mzuri na demokrasia na kupunguza nafasi za watu binafsi, asasi na mashirika.

Rushwa imeenea katika shughuli za serikali kuu na za serikali za mitaa, katika upokeaji mali na taratibu za zabuni za serikali, ugawaji wa ardhi, ukusanyaji wa mapato na uteuzi wa watumishi wa serikali. Malipo ya rushwa yanayotolewa ili kupata huduma za serikali yanainyima nchi mapato ya thamani. Taratibu za zabuni zinazoipandishia bei serikali kama mnunuzi mkuu wa vyakula na huduma huongeza gharama za matumizi ya serikali. Uchunguzi wa uchumi umethibitisha kuwa licha kupandisha bei, rushwa huongeza deni la nchi yoyote inayoendelea na kuongezea gharama za kulipia deni za kila mwaka hapo baadaye. Hatimaye hali hii huishia kushusha viwango, kwani bidhaa duni hutolewa na teknolojia isiyofaa au isiyo ya lazima huagizwa kuendeshea miradi. Maamuzi yanatawaliwa na mtaji, ambao unamnufaisha zaidi mpaliliaji rushwa kuliko matumizi ya watu, ambayo yangekuwa na manufaa zaidi kwa maendeleo. Hatima ya gharama ya rushwa inaweza kuonekana kwenye;

- Kushindwa kufikia malengo ya Serikali
- Uchafuzi wa mazingira
- Kupanda kwa gharama za utawala
- Ukusanyaji kodi duni
- Mmomonyoko wa nguvu za azma ya kushikilia viwango vya juu vya uadilifu;
- Kupunguka heshima ya mamlaka;
- Kupunguka kwa uzalishaji pale muda na nguvu vinapoelekezwa katika kuukamua mfumo badala ya kuendeleza malengo yake;
- Kudhihaki mfumo wa sheria wa nchi;
- Maamuzi kupimwa kwa vigezo vya fedha dhidi ya thamani ya watu au mahitaji;
- Kushuka kwa uwekezaji wa nje

Ni dhahiri, athari za rushwa zinafika mbali na gharama zake kimsingi hazihesabiki. Ni dhahiri pia kuwa ung'oaji kabisa wa rushwa ni lengo la kufikirika tu. Dhamira ya serikali ya Awamu ya Tatu ya kupambana na rushwa

imekuwa haiyumbiyumbi tangu iingie madarakani. Hata hivyo, ni muhimu kabisa kuandaa mikakati inayosisitiza mkabala uliofungamana ili kupunguza na kuzuia kutokea kwa rushwa *uchwara* na rushwa *kabambe* kusikokuwa na sababu.

## 3. MALENGO NA KANUNI ZA MKAKATI HUU

### 3.1 MALENGO

Mkakati thabiti dhidi ya rushwa hauna budi kushikamana na kuchangamana. Hivyo basi mkakati huu unatambua haja ya viongozi wa siasa kuahidi kupambana na rushwa popote pale itokeapo. Unataka kuwa viongozi muda wote wakubali kuchunguzwa. Zaidi ya hayo unalenga zaidi juu ya kukinga matukio ya rushwa ya baadaye kwa kusahihisha athari hasi na kubadili mifumo badala ya kujishughulisha na kutafutana. Mkakati una mtazamo wa kitaifa na wa kisekta katika kulenga.

Mkakati huu, kwa hiyo unaorodhesha malengo ya muda mfupi na malengo ya muda mrefu ya kitaifa, Unashughulikia *kinga, utekelezaji, kuelewesha umma na ujenzi wa taasisi* kwa nia ya kufanikisha yafuatayo:

- Sheria jumlifu dhidi ya rushwa;
- Ugunduzi wa maeneo ya shughuli za serikali yanayoandamwa mno na rushwa na kuzirekebisha;
- Kupata dawa ya rushwa ya kisheria na ya kiutawala ambayo itatoa kizuizi cha kutosha;
- Kujenga ushirikiano mwema kati ya serikali wananchi pamoja na sekta binafsi, mashirika ya weledi, na mashirika ya dini katika kupambana na rushwa.

Malengo ya Muda mrefu

- Ongezeko la ukuaji uchumi katika Tanzania kwa kuimarisha mifumo ya msingi na vikorombwezo;
- Utendeaji sawa wa vikundi tofauti vya kisiasa, kimbari, kidini, na vya kiutamaduni;
- Ongezeko la mapato ya Serikali;

- Uboreshaji wa usawa wa jamii na utulivu;
- Uboreshaji wa ufanisi na uzalishaji katika sekta ya serikali;
- Ongezeko la uwekezaji katika Tanzania;
- Uboreshaji wa welewa wa umma katika jamii na katika sekta ya binafsi.

Malengo ya muda mfupi (mara moja)

Malengo ya mara moja ya mkakati dhidi ya rushwa ni kuhakikisha:

- Matumizi kamili ya raslimali na mali za serikali;
- Usawa wa kupata huduma za serikali za haki za wazi na zenye kukidhi haja.
- Utekelezaji wenye kufaa na wa haki wa shughuli za serikali,
- Upambanaji wa uhakika wa rushwa iliyothibitishwa.

Hususa, mkakati huu utawezesha kufanikisha yafuatayo:

- Kuongezeka kuheshimu utawala wa Sheria kuharakisha utawala mzuri na kukuza uongozi adilifu ndani ya maofisa na mawakala wake.
- Kuimarisha mfumo wa sheria kiasi kwamba haki haitauzwa wala kununuliwa
- Kuwa na Mipango ya kulinda mashahidi wa kujitolea na watoa taarifa
- Uwazi katika serikali na zabuni na mikataba ya kupokea mali.
- Wakala bora na rafiki wa uhamiaji, bandari, forodha na huduma za ushuru.
- Serikali isiyovumilika rushwa kabisa.
- Ujenzi na ukuzaji na kulinda utamaduni wa kujitegemea na uwajibikaji wa pamoja katika mapambano dhidi ya rushwa

- Kuimarisha sera na kunoa kiunzi cha sheria kitakachozuia rushwa.
- Kuimarisha mawakala ya kutekeleza sheria, kwa mfano, ofisi ya Kuzuia Rushwa, Polisi, Ofisi ya Maadili na Tume ya Kudumu ya Uchunguzi.
- Kukuza mahusiano kati ya raia na Serikali katika umoja wa kupambana na rushwa.
- Kujenga ndani ya jamii imani kwamba uwazi na uwajibikaji ni sifa za serikali nzuri na ngao ya lazima dhidi ya rushwa.

## 3.2 KANUNI

### *3.2.1 Kinga*

Kuzuia rushwa kunadai kurahisisha, kuondoa mizengwe, na kutogeuza mipango na taratibu za serikali kuwa mali ya mtu binafsi ili fursa za kutokea rushwa zipunguzwe, Ina maana ya kupunguza au kudhibiti maeneo ya hiari ya mtu. Pale ambapo utaratibu huo unaendelezwa, miongozo wazi iliyoandikwa kwa ajili ya kutumia hiari hiyo sharti ichapishwe. Umma sharti ujulishwe juu ya kuwapo kwa utaratibu unaotoa mapitio ya haraka na imara ya maamuzi tatanishi ndani ya utaratibu wa utawala na sheria.

Kinga inapaliliwa sana pale ambapo watumishi wa serikali *wanalipwa mshahara* unaolingana na mahitaji na matarajio ya wastani. Zawadi kwa ufanikishaji mambo hazina budi kutolewa, na utendaji mzuri kutambuliwa na kuzawadiwa na mifano bora ya utendaji kushangiliwa. Taratibu za kuwashirikisha raia zianzishwe na kuingizwa katika mchakato wa kupitiwa wenye kuendelea. Umma *upimwe baada ya muda* juu ya jinsi wanavyoona mambo yaliyobadilika. Aidha, mapato, mali, na madeni ya maofisa wenye madaraka ya kufanya maamuzi hawana budi *kufuatiliwa barabara kuhakikisha uwiano baina ya mapato yanayojulikana na matarajio ya kadiri.*

Uandaaji wa mfumo wa wazi wenye ushindani halisi, na wa wazi wa kununua mali za umma ni wa lazima. Kuripoti *zawadi zote na takrima* zilizopokelewa zenye thamani zaidi ya kiwango cha chini kilichowekwa wakati mtumishi anatoa huduma za serikali kudaiwe. Kuripoti na kurikodi michango yote ya kisiasa kuwe ni kwa lazima katika kipindi kinachohusika. Pia ni muhimu kupitia na kutekeleza kanuni zinazokingamana kama zinavyotawaliwa na Tume ya Maadili.

Mwisho kuunganisha jitihada za kuunga mkono uzuiaji wa rushwa hakuna budi kujengwa. Miungano hii huleta pamoja sekta binafsi na raia wengine na kuendesha kampeni za *kuuelewesha umma* kupunguza kuvumilia rushwa na kuifanya tendo la hatari kabisa.

### 3.2.2 *Kutekeleza*

Utaratibu huru wa utekelezaji sharti utumiwe na kuimarishwa kuongeza uwezekano wa rushwa kubainiwa na kuadhibiwa . Wachunguzi, washtaki, na mahakimu lazima waweze kutenda kazi zao za kieledi kwa namna ya uhuru ulio wazi na kutekeleza utawala wa sheria dhidi ya wahalifu wote Uwezo tosha wa kuchunguza na kushtaki wenye kupakana na katiba na kanuni za kimataifa za haki za binadamu utakuwa wa lazima.

***Njia za uhakika za kupitishia malalamiko*** lazima ziandaliwe kwa ajili ya wapasha habari ndani ya serikali na uraiani ili kwamba wasijione wameachiwa kulipiziwa kisasi bila sababu.

Utaratibu wa kuwaadhibu wale waliokuwa nje ya mamlaka ya nchi hauna budi kuandaliwa kwa ushirikiano wa kimataifa. Matumizi ya adhabu za kiraia yaimarishwe na kutumiwa kusaidia zilizopo za jinai.

Njia ya *kuorodhesha mashirika yala rushwa* na kutangaza majina yao kama njia ya kuhakikisha nchi nyingine na washindani wanafahamu matendo yao ya rushwa lazima ifuatiliwe.

Taratibu za *kurudisha wahalifu* zifanywe ili maofisa wala rushwa wanaokimbia nchi waweze kurudishwa kwa amri ya mahakama kutoka nchi nzuri sana za makimbilio. Hatua za kisheria hazina budi kuchukuliwa kuwezesha mali za wala rushwa kukamatwa na kufilisiwa, mali hizi ziwe ndani au nje ya nchi.

### 3.2.3 *Kuelewesha Umma*

Umma sharti ueleweshwe kuhusu madhara yanayoletwa na rushwa na kweli kwamba wala rushwa wanaiba mapesa ya umma. Umma unapaswa kuelimishwa juu ya haki zao kuhusu huduma kwa bei iliyowekwa au bure kama hakuna malipo kabisa. Pia wana haja kujua wajibu wao wa kulalamika na taratibu za kufanya hivyo pale maofisa wanapoonyesha tabia za rushwa katika matukio mahususi.

### 3.2.4 *Kujenga Taasisi*

Taasisi zote husika za kutekeleza sheria ambazo ni kitovu cha kupambana na rushwa lazima ziwe na wafanyakazi wa kutosha na wajuzi na vitendea kazi vingine kama zana kali za kupambana na rushwa. Miongozo wazi ya maadili na sheria za kutenda kazi hazina budi kutungwa na kusambazwa. Mafunzo ya kuendelea lazima yatolewe kwa watumishi wote wa serikali katika ngazi zote.

Mifumo ya ndani ya kushughulikia fedha lazima ipitiwe kuhakikisha utoshelezaji na kufaa kwake. Halmashauri kuu ya Zabuni na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu lazima waongeze uangalifu kama mawakala wasimamizi huru wa shughuli za mikataba ya serikali na zabuni za umma na ununuzi wa mali. Ununuzi lazima uwe weledi kwa kuhakikisha kuwa kote katika ngazi ya serikali kuu na ya serikali za mitaa watumishi wajuzi na waaminifu wanaajiriwa. Utendaji bora na mifumo ya uwazi lazima vishikiliwe muda wote.

Watoa maamuzi sharti wateuliwe bila kutabiri ni nani atahusika katika zoezi fulani maalum. Maamuzi ya haraka yasisitizwe kuondosha ucheleweshaji unaowezesha rushwa kutendeka.

## 4. UTASHI WA KISIASA

Ili kupata mkakati endelevu na wa uhakika dhidi ya rushwa utashi wa kisiasa ni mwanzo muhimu na mkuu kabisa. ***Utashi wa Kisiasa*** unamaanisha nia inayodhihirishwa na watendaji wa kisiasa kama ilivyo katika Tanzania kushambulia sababu na athari za rushwa zinazofahamika katika ngazi ya mfumo. Rushwa hii inalenga kwenye mazingira yanayohusisha watawala rasimu wasomi, wanasiasa, wafanyabiashara na wafanyakazi katika kufuja fedha za umma kwa kiwango kikubwa kwa njia mbalimbali za mashakamashaka. Kuwako kwa ***Utashi wa Kisiasa*** kunawezesha kutunga sheria inayofaa na kuunda miundo asasi fanisi ya kupambana na rushwa.

Utashi wa Kisiasa katika mapana yake unahusisha sekta binafsi na wananchi kwa utashi na matendo yao pamoja kushinda mifumo ya rushwa. Ni uwezo wa kupanga na kuweka aula miongoni mwa changamoto kadha zinazo sababishwa na rushwa. Unahusu kujenga uhalali, uaminifu, na kuungwa mkono na wengi kisiasa na utii katika jamii na ndani ya serikali. Utashi wa Kisiasa upo hapa lakini changamoto kubwa kabisa ni kuthibitishia jamii beuzi kuwa mkakati huu ni aminifu na halisi. Kama ilivyokwishatajwa mapema mkabala wa kubadili kwa yaliyotangulia ni wa muhimu sana.

Mkakati huu unategemea kuwako kwa utashi wa kisiasa. Hali kadhalika mtaji wa kutosha utahitajika na kutolewa kuwezesha utekelezaji wake kulingana na uwezo wa Serikali wa kifedha. Pia unatarajiwa kuwa washiriki ambao pia wana hamu kubwa kuona jamii iliyojikomboa na rushwa katika Tanzania watatoa mchango wao wa kusaidia utekelezaji wake. Msaada kutoka kwa wananchi, vyombo vya habari, na sekta binafsi unatambuliwa kuwa ni wa lazima katika kufanikisha utekelezaji wa mkakati dhidi ya rushwa.

## MAENEO SABA YA AULA ZA MKAKATI

### 5.1 Utawala wa Sheria na Mfumo wa Kisheria

Kipengee hiki kinakusudiwa kusaidia mapitio ya sheria za sekta na kuandaa masharti ya lazima katika kurudisha imani ndani ya mfumo wa sheria na mawakala ya kutekeleza sheria.

### 5.2 Nidhamu na usimamizi wa fedha

Imekusudiwa kupunguza na kuondosha ulaji wa fedha za umma na watumishi wasiokuwa waaminifu na kuongeza ukusanyaji wa mapato kuwezesha kulipia huduma za jamii na kusaidia kukua kwa uchumi.

### 5.3 Kununua

Kushikilia imara taratibu za uwazi katika kuendesha zabuni na manunuzi.

### 5.4 Kuelimisha Umma Kutambua na kujua haki zao

Kuandaa mipango ya elimu na kufanya watu wafahamu jinsi rushwa inavyoumiza uchumi na hatimaye kugeuza misingi na thamani za jamii.

### 5.5 Kurekebisha Utumishi wa Serikali (Kujenga Uwezo)

Kutambua kuwa maofisa wa Serikali si "mabwana" bali "watumishi" wanaowajibika kwa matendo yao na kwa hiyo, wanastahili malipo maridhwa.

### 5.6 Watoa habari na Ulinzi wa Mashahidi

Kutambua kuwa watoa habari na raia wanaojitokeza katika vyombo vya kutekeleza sheria kuripoti matukio ya rushwa hawana ulinzi. Mpango utaandaliwa kufanikisha jambo hili. Nia ni kuwakinga na kueneza mpango kabambe ambao utawapa moyo raia kushiriki.

### 5.7 Vyombo vya Habari

Kuripoti wanaojihusisha na rushwa bila woga wala upendeleo na kutangaza madhara wanayowafanyia watu wasio na hatia, maskini na wanyonge katika Tanzania.

6. Yafutayo ni mambo muhimu katika utekelezaji wa mkakati huu:

- **Kibali cha Kisiasa cha Mkakati**

Ni muhimu sana kuona kuwa kutekeleza kwa mkakati huu kunaungwa mkono sana na Rais wa Serikali na kwamba sera ya kuchukua hatua kali dhidi wanasiasa na mameneja katika sekta ya utumishi wa serikali itatekelezwa.

- **Mtaji wa Kutekelezea**
  **Mtaji wa nchini**

Kuhakikisha utekelezaji barabara wa mkakati dhidi ya rushwa ni sharti Serikali ya Tanzania itenge fedha ya kutosha kwa ajili ya asasi zinazohusika na utekelezaji wa shughuli.

- **Msaada wa Jumuiya ya Wafadhili**

Kwa kuzingatia hali ya sasa ya uchumi wa Tanzania ni dhahiri kuwa serikali inahitaji msaada kutoka jumuiya ya wafadhili kama inataka kufanikiwa katika utekelezaji wa mkakati dhidi ya rushwa. Ahadi za uhakika zinatakiwa kutoka mawakala wa wafadhili kadhaa wa nchi na nchi na wa nchi nyingi kusaidia utekelezaji wa mkakati.

- **Msaada wa Raia na Vyombo vya Habari**

Ushirikishaji wa raia na vyombo vya habari katika maandalizi na utekelezaji ni muhimu kwa ufanisi wa mkakati kwa kuwa wana dhima muhimu katika kuwafahamisha raia na kuwabaini wala rushwa.

- **Msaada wa Sekta Binafsi**

Kushirikisha kikamilifu sekta binafsi katika kuandaa na kutekeleza mkakati huu kutasaidia kupunguza "upande wa ugavi" wa rushwa na kubaini wala rushwa katika utawala wa serikali.

- **Mipango ya kurekebisha Serikali za Mitaa na Utumishi wa Serikali**

Uhusiano wa kudumu baina ya Mipango ya Kurekebisha Serikali za Mitaa, Mipango ya Kurekebisha Utumishi wa Serikali na Mipango ya Kurekebisha Sekta ya fedha na ya Sheria unachangia mkakati dhidi ya rushwa na kuzaa utawala nzuri.

## 7. MAMBO YANAYOCHOCHEA UENDELEZAJI MKAKATI

### 7.1 Kuunga mkono Sera

Kuendelea kutambua na kuunga mkono mkakati huu ni muhimu kwa uendelezaji wake wa muda mrefu. Serikali imetangaza sera dhidi ya rushwa ikiunga mkono hatua zitakazochukuliwa chini ya mkakati huu. Sera hii itafasiriwa katika mpango wa utendaji kufuatana na aula kama ilivyopangwa ndani ya dama.

### 7.2 Teknolojia Muafaka

Ujenzi wa mifumo imara na ya wazi inategemea teknolojia ya kompyuta iliyopo na programu zilizopo na zinazotengenezeka nchini. Jumuiya ya wafadhili itatakiwa kuongezea katika teknolojia iliyopo kwa utekelezaji mzuri wa mkakati huu.

### 7.3 Uwezo wa Kitaasisi na Kiuongozi

Kuweka uwezo unaofaa wa kiasasi na wa kiuongozi ni sehemu ya mradi (taz. Matokeo 1 na 3)

### 7.4 Sababu za Kijamii-Kiuchumi

Utekelezaji wa mkakati dhidi ya rushwa utakuwa na matokeo ya kijamii na ya kiuchumi kwa watumishi wa serikali wa ngazi za chini na waajiriwa wengine waliojiingiza katika rushwa uchwara ili kupata kipato cha kujikimu. Ujira wa kutosha lazima upatikane unaolingana na gharama za kuishi. Marekebisho ya utumishi wa serikali yanashughulikia suala hili haraka iwezekanavyo ili mkakati huu uwe na maana.

### 7.5 Vipengee Vya Kijinsia

Mkakati dhidi ya rushwa unakabili idadi kadha ya matendo ya kirushwa yaliyodhamiriwa kuwadhalilisha wafanyakazi wa kike, wanafunzi na wateja wa huduma za serikali.

### 7.6 Uwezo wa Kifedha

Faida za muda mrefu za kiuchumi kutokana na utekelezaji wa mkakati wa ongezeko la mapato na upunguaji wa matumizi kwa serikali zitazidi sana

gharama za kutekeleza mkakati. Hata hivyo kwa kipindi kifupi serikali itahitaji msaada wa kifedha kutoka kwa jumuiya ya wafadhili kuhakikisha kuanzishwa utekelezaji wa mara moja na imara wa shughuli za mkakati.

## 8. UTEKELEZAJI WA MKAKATI

Utekelezaji wa mkakati huu umeonyeshwa chini ya matokeo ya 6 sehemu ya 10 ya waraka huu na katika mpango kinaganaga wa utekelezaji tangu ukurasa wa 14 hadi 30 na katika kiambatisho 1.

Jukumu kuu la kuratibu mkakati litakuwa la Waziri wa Nchi, Utawala Bora katika ofisi ya Rais, Katibu Mkuu na Maofisa Watendaji Wakuu katika Wizara, asasi na mashirika yanayohusika watakuwa watendaji wakuu wa sera.

## 9. UFUATILIAJI NA TATHMINI

Mfumo wa aina moja wa kuripoti utakuwa kupitia kwa Waziri wa Utawala Bora kurahisisha ufuatiliaji wa karibu wa mafanikio ya malengo na utekelezaji wa shughuli za mkakati.

## 10. MATOKEO

***Tokeo la 1: Utoaji wa huduma bora na zenye kujali mteja za Serikali kuhakikishwa***

Moja ya mambo ya msingi yenye kuathiri ubora wa huduma na ufanisi wa huduma za Serikali ni kiwango cha kujitolea na uhodari cha watumishi wa serikali na watumishi wengine walioajiriwa na serikali kuhudumia umma na jumuiya ya wafanya biashara. Tokeo hili linakusudia kuhakikisha viongozi, watumishi wa serikali, waajiriwa wengine na watu binafsi na makampuni yaliyopewa mkataba wa kutoa huduma za umma wanatekeleza kazi zao kwa njia ya uhodari na ubora wakizingatia kanuni za utendaji na viwango vya maadili yaliyowekwa kwa huduma za serikali. Utekelezaji wa shughuli zilizoorodheshwa chini ya tokeo hili sharti uratibiwe kwa karibu sana na shughuli zitakazoendeshwa chini ya marekebisho ya sekta ya huduma za serikali.

Hatima ya tokeo hili inatarajiwa kuwa kiwango cha juu zaidi cha raia kuridhishwa na huduma zitolewazo na mawakala wa serikali na mashirika ya umma.

***Tokeo 2: Mifumo thabiti na ya wazi, taratibu, sheria na miongozo kuwekwa***

Karibu mifumo yote, taratibu na miongozo iliyopo imepitwa na wakati, tatanishi na isiyozaa matunda, yenye kusababisha ucheleweshaji mwingi na kutoa mwanya wa matendo ya rushwa. Tokeo hili linakusudia kudurusu taratibu, sheria na miongozo ya kirasimu tatanishi iliyopo ili kuharakisha kutoa huduma na kuondosha "urasimu".
Wakati huo huo tokeo litaweka taratibu na miongozo wazi na safi katika maeneo ambayo yanaruhusu matendo ya rushwa, uendeshaji mbaya na matumizi mabaya ya madaraka. Tokeo pia linakusudia kuweka kiwango cha juu cha uwazi ndani ya mifumo, taratibu, sheria na miongozo ili kuwezesha wananchi kupata maarifa bora juu ya kile wanachoweza kutarajia kwa huduma zinazotolewa, mahitaji na viwango.

*Hatima ya tokeo hili itakuwa ni imani bora ya wanachi kwa mawakala ya Serikali na mashirika ya umma.*

***Tokeo la 3: Uwezo wa Kitaasisi na wa Kiuongozi wa kutoa huduma safi na za wazi kujengwa***

Karibu Mawakala na mashirika ya umma ya Serikali ya Tanzania yote yaliibuka kutokana na mfumo wa kikoloni au yalianzishwa miaka ya sabini na ya themanini kusaidia mfumo tofauti wa siasa. Baada ya muda mrefu karibu yote yamegeuka kuwa mashirika rasimu sana na zembe yakitoa nafasi kwa matendo ya rushwa na yasiyo na haki wala usawa. Tokeo hili linakusudia kuhakikisha kuwa asasi za umma zina uwezo wa kiasasi na wa kiuongozi unaofaa wa kutekeleza mkakati dhidi ya rushwa na kutoa huduma za umma nyingi bora kama inavyotakiwa na serikali.

Tokeo pia linakusudia kujenga uwezo wa asasi za umma ambazo zimekabidhiwa kazi ya kuratibu kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa mkakati dhidi ya rushwa. Tokeo ni pamoja na shughuli za kufanya tathmini ya miundo ya kiuongozi usimamizi wa upangaji na uwezo wa uendeshaji, raslimali na vikorombwezo.

***Tokeo la 4: Kuweka Kiunzi cha Kisheria na cha Kiutawala kuhakikisha utendaji wa uhakika, sawa, wa haki na wa wazi***

Mahakama na mfumo wa sheria ndio uti wa mgongo katika jitihada za serikali za kuhakikisha haki sawa na kuwatendea kwa uadilifu wananchi wote nchini. Hata hivyo, sheria zilizopitwa na wakati na maagizo na kanuni zisizokuwa wazi na tatanishi vimefanya mfumo wa sheria usiwe fanisi na kuzongwa na matendo ya rushwa. Tokeo hili linakusudia kupitia na kugeuza mfumo wa sheria na wa utawala kuwa wa kisasa ili kuakisi sera ya serikali ya utendeaji wananchi wazi, sawa, adilifu na thabiti na utoaji wa huduma kwa wananchi. Tokeo pia lina shughuli zinazokusudiwa kuanzisha kiunzi chenye vifungu vya kisheria na vya kiutawala vya kuwazuia viongozi na watumishi wa serikali pamoja na watu binafsi, na makampuni kushiriki katika matendo ya rushwa. Hatima ya tokeo hili inayotarajiwa ni utendeaji fanisi, sawa na adilifu zaidi wananchi na jamii ya wafanyabiashara mahakani na katika mfumo wa sheria.

***Tokeo la 5: Umma kufahamu maono, haki, viwango, miko ya utendaji iliyowekwa***

Katika jamii nyingi za kiraia ubaridi na kutoamini asasi za serikali na viongozi wa umma vinatawala. Moja ya sababu kuu zinazochangia hali hii ni ukosefu wa maarifa ya haki, taratibu, viwango na miko ya kutenda kazi wanavyotarajiwa kuwa navyo viongozi wa kisiasa na watumishi wa serikali. Tokeo hili linakusudia kusambaza habari kwa wananchi juu ya haki, viwango vya huduma, taratibu, sheria, kanuni na njia za habari na malalamiko Shughuli zake ni pamoja na kutekeleza kampeni za kuelewesha na kufuatilia, na kufanya tathmini ya kiwango cha welewa. *Hatima ya tokeo hili inayotarajiwa ni kushiriki kwa wingi kwa jamii ya kiraia katika kuhakikisha utendeaji na utoaji wa huduma za haki, sawa na mawakala ya serikali na mashirika ya umma.*

***Tokeo la 6: Uhakikishwaji wa utekelezaji barabara wa mkakati dhidi ya rushwa.***

Ufanikiwaji wa mkakati wa Serikali dhidi ya rushwa unategemea kwa kiasi kikubwa juu wa uwezo wa asasi zinazohusika na uwezo wa mawakala kupanga, kuratibu na kusimamia utekelezaji wa sehemu mbalimbali za mkakati. Shughuli zinazopelekea kufanikiwa kwa tokeo hili zinalenga juu ya kujenga mchakato imara wa aina moja kwa kupanga na kutekeleza mkakati. Linaandaa muundo wa kutumia mifumo ya kuratibu shughuli kwa aina moja na ufuatiliaji na usimamizi thabiti wa mchakato.

*Hatima ya tokeo hili litakuwa kwamba kila taasisi na wakala wa umma itakuwa na mpango wa aina moja wazi na thabiti wa utendaji wa kutekeleza mkakati dhidi ya rushwa.*

## II. MPANGO WA UTEKELEZAJI JUMUIFU NA TONDOTI

# (DAMA) LA MPANGO JUMUIFU NA TONDOTI WA UTEKELEZAJI

| TATIZO | WIZARA (Idara) | NANI ANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA TEKELEZWA AC=dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA LINI (1) muda mfupi Des. 2000 (2) muda wa kati 2005 (3) muda mrefu: enye kuendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| 1. ALA WA SHERIA NA KIUNZI CHA KISHE-RIA | • Mahakama<br>• PCB<br>• Polisi<br>• DPP<br>• Sheria na mambo ya Katiba | Mla rushwa | Mtu asiyehusika, Maskini na Mnyonge | • Kuacha kazi kunako endelea kwa maofisa watekeleza sheria na mahakimu na baadaye kushikwa kufunguliwa mashtaka ya jinai<br>• Kuanzishwa Bodi ya sheria ya Nidhamu<br>• Kuanzishwa mahakama ya Biashara<br>• Mradi wa majaribio katika aina nyingine ya kusuluhisha magomvi (ADR)<br>• Maeneo ya matatizo kuainishwa (Film up)<br>• Kurekebisha mara kwa mara sheria kuchukuana na mazingira yanayobadilika yenye kupalilia rushwa | • Kuimarisha Mahakama (yote vikorombezo + wafanyakazi waliofunzwa)<br>• Kuimarisha mawakala ya kutekeleza sheria (Polisi, ofisi ya vita dhidi ya rushwa na DPP)<br>• Kupandisha mshahara na pensheni kwa mahakama ya watekelezaji wa sheria.<br>• Kurekebisha Katiba kuingiza uundaji wa Tume ya Haki za Binadamu | • Kuanzisha elimu ya umma juu ya haki za kisheria za raia.<br>• Hamasisha kwa ADR, suluhisho kupatanisha na kuafikiana badala ya mashtaka.<br>• Msaada wa Sheria kwa maskini<br>• Kuweka utaratibu ambao kwao hatua zinaweza kuchukuliwa wala rushwa<br>• Kuweka bodi za usimamizi katika ngazi mbalimbali za polisi na za mahakama | • Kuwezesha utoaji halali wa Haki (1)<br>• Kupunguza "sheria mkononi" (2)<br>• Kupunguza mashtaka yasiyo ya lazima na kupunguza ucheweleshaji katika kutoa huduma za sheria (2)<br>• Kurudisha imani katika mfumo wa sheria (3).<br>•kuongezeka uhalali wa serikali. |

| TATIZO | WIZARA (Idara) | NANI ANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA TEKELEZWA AC=dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA LINI (1) muda mfupi Des 2000 (2) muda wa kati 2005 (3) muda mrefu: enye kuendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| | | | | • Kutambua sheria zilizopitwa na wakati<br>• Sheria za kupitiwa kuainishwa na kupangiwa aula<br>• Sheria isiyofaa iliyomo ndani ya Sheria ya Kuzuia Rushwa inarekebishwa. | • Kuruhusu kutenganisha madaraka ya Jaji Mkuu na rais wa Mahakama ya Rufaa<br>• Kuwezesha kurekebisha Katiba na kuweka mpaka wa wazi wa kazi na madaraka baina ya wanasiasa na watumishi wa serikali.<br>• Kujenga hoja ya kusikiliza maoni ya umma<br>• Kuandaa warsha kushughulikia haki za kisheria za wananchi | | |

## (DAMA) LA MPANGO JUMUIFU NA TONDOTI WA UTEKELEZAJI

| TATIZO | WIZARA (Idara) | NANI ANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA TEKELEZWA<br>AC=dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA LINI<br>(1) muda mfupi Des. 2000<br>(2) muda wa kati 2005<br>(3) muda mrefu: enye kuendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| 1. ALA WA SHERIA NA KIUNZI CHA KISHE-RIA | • Mahakama<br>• PCB<br>• Polisi<br>• DPP<br>• Sheria na mambo ya Katiba | Mla rushwa | Mtu asiyehusika, Maskini na Mnyonge | • Kuacha kazi kunako endelea kwa maofisa watekeleza sheria na mahakimu na baadaye kushikwa kufunguliwa mashtaka ya jinai<br>• Kuanzishwa Bodi ya sheria ya Nidhamu<br>• Kuanzishwa mahakama ya Biashara<br>• Mradi wa majaribio katika aina nyingine ya kusuluhisha magomvi (ADR)<br>• Maeneo ya matatizo kuainishwa (Film up)<br>• Kurekebisha mara kwa mara sheria kuchukuana na mazingira yanayobadilika yenye kupalilia rushwa | • Kuimarisha Mahakama (yote vikorombezo + wafanyakazi waliofunzwa)<br>• Kuimarisha mawakala ya kutekeleza sheria (Polisi, ofisi ya vita dhidi ya rushwa na DPP)<br>• Kupandisha mshahara na pensheni kwa mahakama ya watekelezaji wa sheria.<br>• Kurekebisha Katiba kuingiza uundaji wa Tume ya Haki za Binadamu | • Kuanzisha elimu ya umma juu ya haki za kisheria za raia.<br>• Hamasisha kwa ADR, suluhisho kupatanisha na kuafikiana badala ya mashtaka.<br>• Msaada wa Sheria kwa maskini<br>• Kuweka utaratibu ambao kwao hatua zinaweza kuchukuliwa wala rushwa<br>• Kuweka bodi za usimamizi katika ngazi mbalimbali za polisi na za mahakama | • Kuwezesha utoaji halali wa Haki (1)<br>• Kupunguza "sheria mkononi" (2)<br>• Kupunguza mashtaka yasiyo ya lazima na kupunguza ucheweleshaji katika kutoa huduma za sheria (2)<br>• Kurudisha imani katika mfumo wa sheria (3).<br>•kuongezeka uhalali wa serikali. |

| TATIZO | WIZARA (Idara) | NANI ANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA TEKELEZWA AC=dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA LINI (1) muda mfupi Des 2000 (2) muda wa kati 2005 (3) muda mrefu: enye kuendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| | | | | • Kutambua sheria zilizopitwa na wakati<br>• Sheria za kupitiwa kuainishwa na kupangiwa aula<br>• Sheria isiyofaa iliyomo ndani ya Sheria ya Kuzuia Rushwa inarekebishwa. | • Kuruhusu kutenganisha madaraka ya Jaji Mkuu na rais wa Mahakama ya Rufaa<br>• Kuwezesha kurekebisha Katiba na kuweka mpaka wa wazi wa kazi na madaraka baina ya wanasiasa na watumishi wa serikali.<br>• Kujenga hoja ya kusikiliza maoni ya umma<br>• Kuandaa warsha kushughu-likia haki za kisheria za wananchi | | |

| TATIZO | WIZARA (Idara) | NANI ANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA TEKELEZWA AC=dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA LINI (1) muda mfupi Des. 2000 (2) muda wa kati 2005 (3) muda mrefu: enye kuendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| | | | | | • Kuanzisha ukaguzi changanuzi juu ya polisi Mahakama, Ofisi ya Mwana - Sheria Mkuu (AG) kwa ubingwa uliogharimiwa na Benki ya Dunia.<br>• Kutumia sheria, amri, taratibu na kanuni zote za kudumu.<br>• Kupitia zaidi sheria na taratibu za kutunga sheria.<br>• Kupitia Kanuni za Utumishi wa Serikali, Taratibu za Nidhamu na Amri za kudumu na kuchapisha upya | | |

| TATIZO | WIZARA (idara) | NANI ANANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA TEKELEZWA AC=dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA LINI<br>(4) Muda mfupi Des. 2000<br>(5) Muda wa kati 2005<br>(6) muda mrefu enye kuendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| 2. NIDHAMU YA FEDHA NA UENDESHAJI | • Wizara ya Fedha.<br>• Kurugenzi za fedha za Wizara zote<br>• Benki Kuu ya Tanzania<br>• Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA)<br>• Forodha<br>• Mamlaka za leseni<br>• Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG). | • Mla rushwa | Mtu asiyehusika Maskini na mnyonge | • kuanzisha Kodi ya ongezeko la thamani (VAT)<br>• Kuundwa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania.<br>• Benki ya Serikali ya Taifa ya Biashara kubinafsishwa na wadeni kulazimishwa kulipa madeni<br>• Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali kupewa mtaji mkubwa zaidi.<br>• Kupunguza madaraka ya hiari katika ukadiriaji wa kodi na ushuru | • Kuendesha mfumo wa ukaguzi wa ndani na nje wa mara kwa mara<br>• Kukuza ufundi maalum katika CID (Idara ya Uchunguzi wa Jinai) na DPP (Ukurugenzi wa Mashirika ya Umma) katika Maeneo ya uhalifu wa kiuchumi na wa vikundi vilivyoandaliwa.<br>• kuasisi utaratibu wa wazi wa kusikiliza ripoti za (CAG) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali. | • Unda muungano kwa hadhari juu ya vipengele vyote vya mahesabu ya umma na vya uendeshaji wa fedha za umma<br>• Unda kikosi cha shinikizo kufuatilia kwa mfano, matokeo ya ukaguzi wa CAG<br>• Anzisha stadi za kufatilia migao ya bajeti katika sekta fulani zikiambatana na data halisi. | • Ukusanyaji bora wa mapato (1)<br>• Upunguaji wa unyonyaji wa fedha za umma (2)<br>• Ugawaji bora wa mitaji ya kifedha kwa mawakala wa serikali ya kutoa huduma za umma (2).<br>• Uwezo wa kutoa masharti sawa ya malipo kwa watumishi wa serikali - (3).<br>• Zikua makosa Kiuhasibu (2) Shikilia nidhamu ya kifedha - (3). |

| TATIZO | WIZARA (idara) | NANI ANANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA TEKELEZWA AC-dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA LINI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| | | | | • Kuingiza mfumo changamani wa fedha na uendeshaji wenye kutumia kompyuta katika asasi za umma zote.<br>• Kuendelea kurahisisha kodi na kutoa taarifa za kodi kwa wananchi.<br>• Kuboresha mishahara ya watumishi wa Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA).<br>• Kutoa mkataba kwa makampuni ya ukaguzi wa shehena kabla ya kusafirishwa | • Kuweka rekodi za fedha, za masjala na ripoti fanisi na salama.<br>• kutoa misingi ya Kisheria na taratibu za kudhibitiwa misamaha ya hiari ya kodi<br>• Kukuza mazungumzo baina ya vyombo vya serikali na raia juu ya uendeshaji wa fedha.<br>• Kuanzisha ukaguzi changanuzi juu ya kazi ya TRA na CAG kwa ubingwa uliogharimiwa na Benki ya Dunia. | | |

| TATIZO | WIZARA (idara) | NANI ANANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA TEKELEZWA AC=dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA LINI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| | | | | • Kunyoosha sheria ya kodi (Sheria Na. 277 ya 1997)<br>• Kurahisisha Leseni ya Biashara ya Madini (Sheria ya Madini 1998).<br>• Kikosi cha Kazi cha kupitia sheria ya Kodi ya Mapato. | • Oanisha kodi juu ya mazao ya madini na mafuta na nchi za jirani.<br>• Pitia kodi za moja kwa moja na zisizokuwa za moja kwa moja kuhusu mazao ya mafuta.<br>• Zuia magendo, biashara haramu na maduhuli haramu.<br>• Dhibiti vikali misafara ya kupita<br>• Kurekebisha ushuru na kupanua msingi wa kodi.<br>• Tumia ufundi wa GATT wa kuthaminii.<br>• Kuoanisha utaratibu wa rufani za kodi. | | |

| TATIZO | WIZARA (Idara) | NANI ANUFAIKA | NANI ANAPOTE-ZA | MAMBO YALIYOKWISHA TEKELEZWA AC=dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARA-JIWA NA LINI (7) muda mfupi Des 2000 (8) muda wa kati 2005 (9)muda mrefu: enye kuendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| 3.KUNU-NUA | • Bodi kuu ya zabu-ni<br>• wizara ya Ka-zi<br>• Wizara ya Uli-nzi<br>• Wizara nyingine zote<br>• Fedha za Pe-nsheni<br>• Bodi za usa-jili wa kiel-edi | • Mpitisha maamuzi mla rushwa na mgavi/mtoa zabuni asiyekuwa mwaminifu | Mgavi / mtoa zabuni mwaminifu na raia | • Kusawidi Sheria mpya ya kununua na kanuni<br>• Kuboresha ufuatiliaji wa taratibu za (kuomba) zabuni ndani ya Bodi za Zabuni Kuu na za mikoa pamoja na kamati za Kiwizara<br>• Kubadilisha wajumbe katika Bodi za serikali za kununua na za kutoa zabuni.<br>• Ufuatiliaji wa karibu wa vyanzo vya bei/ zabuni zilizopok-elewa.<br>• Kuanzisha "sanduku" la kuwekea zabuni/bei<br>• Zabuni/bei halali kufungwa kwa lakiri na kufunguliwa na kamati ya zabuni tu. | • Kuidhinisha / pitisha sheria<br>• Kufuatilia na kubadilisha wala rushwa kuendelea<br>• Kuunda kada ya Wanunuzi stadi katika Bodi Kuu na za Mikoa, pamoja na ndani ya kamati za zabuni za Wizara<br>• Kipindi cha mjumbe wa Bodi za zabuni kuwa na kikomo.<br>• Kutangaza hadharani matokeo ya zabuni. | • Toa maoni yaliyochunguzwa vyema juu ya utoaji wa zabuni zote kupitia muungano wa mabingwa wa ununuzi.<br>• Andaa warsha za raia juu ya taratibu za kununua.<br>• Ukaguzi wa kina wa mikataba ya serikali na watumishi, wanaotoa na viwanda<br>• Fuatilia mchakacho wote wa zabuni na kutoa bei za zabuni<br>• Tayarisha warsha za kushirikisha kwa maafikiano na uamuzi wa pamoja katika manunuzi. | • Kushusha bei za zabuni kwa bidhaa na huduma (1)<br>• Kupunguza matumizi ya umma katika bidhaa na huduma. (1)<br>• Wagavi/watoa zabuni waaminifu watakuwa na hali bora kifedha (2)<br>• Kukuza ushindani kutokana na uwazi (2)<br>• Iktisadi katika manunuzi ya Serikali (3)<br>• Utoaji wa haki wa mikataba (3)<br>• Kuongezeka uwazi katika taratibu za zabuni (3) |

| TATIZO | WIZARA (Idara) | NANI ANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA TEKELEZWA<br>AC=dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARA-JIWA NA LINI<br>(7) muda mfupi Des 2000<br>(8) muda wa kati 2005<br>(9)muda mrefu: enye kuendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| | | | | • Vifaa vya ofisi kupatikana toka bohari za serikali, Idara au mawakala walioteuliwa.<br>• Bodi za usajili wa makontrakta na wa-shauri kuundwa. | • Anzisha utaratibu wa rufaa kuhusiana na ugawaji wa zabuni.<br>• Tangazia umma sababu njema ya uwekezaji wa miradi mikuu ya kiuchumi.<br>• Tangaza mikataba yote ya matokeo muhimu.<br>• Punguza uingiliaji (wa) kirasimu katika ununuzi.<br>• Punguza taratibu za manunuzi ya vitu vya thamani ndogo.<br>• Andaa mikutano ya mara kwa mara ya wazi kati ya wanajopo kutokana na wafadhili , raia, sekta binafsi na kamati za zabuni za Serikali Kuu, za Mikoa na za Wizara.<br>• Tayarisha orodha ya wakorofi miongoni mwa wagavi wa bidhaa na huduma.<br>• Zabuni zote kutangazwa wazi magazetini. | | • Kuongezeka ufanisi katika manunuzi kwa kupunguza kabisa maingilio ya kirs imu (3)<br>• Udanganyifu kidogo katika misamaha na kutoa mikataba (2) |

| TATIZO | WIZARA (idara) | NANI ANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA-TEKELEZWA AC- dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA LINI<br>(10) Muda mfupi Des. 2000<br>(11) muda wa kati 2005<br>(12) muda mrefu. enye kuendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| 4. KUUELEWESHA NA KUUHADHARISHA UMMA JUU YA HAKI ZAO | • PCB<br>• Vyombo vyote vya habari<br>• Wizara zote<br>• Vikundi vyote visivyokuwa vya serikali<br>• Vyama vyote vya wananchi | Mla Rushwa | Mtu asiyehusika maskini na mnyonge | • Kusambaza Ripoti ya Warioba maktaba zote nchi nzima (Kiswahili na Kiingereza)<br>• Utangazaji zaidi wa matukio ya rushwa katika vyombo vya habari<br>• Kipindi cha Juma cha redio (kila Jumamosi) na Radio Tanzania Dar es Salaam (RTD)<br>• Idara ya Serikali Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NGO), Vyama | • Kufuatilia mkakati wa Kitaifa dhidi ya Rushwa Tanzania<br>• Kukagua utoaji wa huduma ili kufanya tathmini ya uthabiti wa hatua dhidi ya rushwa<br>• Kuendesha warsha ili kukutanisha Wananchi na sekta binafsi kuingiza mkakati wa Kitaifa dhidi ya Rushwa katika sehemu zake zinazoathiri haki za msingi zote kwa njia ya mshikamano na ubia.<br>• Tafsiri kwa Kiswahili sheria za ardhi na sheria nyingine zinazoathiri haki za msingi | • Kuimarisha Uanzishaji wa Vyama vya Wananchi vyenye ajenda ya wazi ya kupambana na rushwa<br>• Vyama visivyo vya serikali (NGO) kushiriki katika mipango ya wazee dhidi ya rushwa<br>• Kuanzisha miradi ya kufunza wenyekujitolea kuendesha kampeni dhidi ya rushwa kusambaza habari katika jitihada dhidi ya rushwa.<br>• Endesha vikundi vya sanaa za | • Jamii iliyoelimika (1) (2) na (a)<br>• Kutovumilia rushwa kabisa (3)<br>• Geuza rushwa toka zoezi la hatari ndogo hadi zoezi la hatari kubwa (3)<br>• Warsha katika Dar es Salaam mwezi Septemba 1999 (1).<br>• Pokea yasemwayo na kuyawasilisha katika warsha za baadaye (2) (3) viwango vya kukuza viwango vya maadili vya uraia na vya wema na ubaya (3).<br>• Kuza picha bora ya utawala mzuri, fanisi na uliojikomboa na rushwa (2). |

| TATIZO | WIZARA (idara) | NANI ANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA-TEKELEZWA AC=dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA LINI (10) Muda mfupi Des. 2000 (11) muda wakati 2005 (12) muda mrefu: enye kuendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| | | | | vya Wananchi n.k. kuombwa kujaza dama la hatua dhidi ya rushwa zilizopendekezwa.<br>● Andiko la Mkakati wa Kitaifa dhidi ya rushwa (A-C) Tanzania kumalizika. | ● Chapa mabango na vibrasha kutangaza haki za wananchi na kulaani rushwa katika umbile lake lote.<br>● Kuitisha mikutano ya waandishi wa habari juu ya matukio makuu yanayoathiri sekta ya umma.<br>● Kutangaza dosari za ukaguzi (wa mahesabu). | maonyesho na kuvitumia kuendesha mfuko na kuvielekeza kukuza elimu ya uraia.<br>● Kudai viongozi katika serikali na katika sekta za Biashara kutangaza mali zao. | Amsha ari ya uraia bora kwa kuhimiza umma kuripoti rushwa bila woga wa kulipizwa kisasi |

| TATIZO | WIZARA (idara) | NANI ANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA-TEKELEZWA AC=dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA LINI (13) Muda mfupi Des. 2000 (14) muda wakati 2005 (15) muda mrefu: enye kuendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| 5. KUREKE-BISHA UTUMISHI WA SERI-KALI | • PCB<br>• Mahakama<br>• Polisi<br>• TRA<br>• Wizara zote<br>• Mamlaka zote za Serikali<br>• Mashirika yote ya umma | Watumishi wa serikali Waandamizi wala rushwa na viongozi wa biashara wasio na murua | • Watumishi wa serikali waaminifu na viongozi wa biashara wasiosalimu amri | • Kung'oa wala rushwa serikalini<br>• Ubinafsishaji unaoendelea<br>• Kuanzisha mabadiliko ya malipo mifumo ya pensheni n.k.<br>• Kutunga sheria ya pensheni kwa watumishi wa serikali katika Februari 1999-12-13<br>• Kuanza kurekebisha Kanuni Kuu<br>• Kugatua kunakoendelea<br>• Upitiaji wa mifumo na upangaji upya unaoendelea. | • Kukamilisha tendo la ubinafsishaji wa maana<br>• Kuepuka kuteua tena maofisa wala rushwa<br>• Orodhesha vikundi vya biashara vila rushwa<br>• Lipa mshahara wa kuwezesha kuishi na kutoa masharti bora ya kustaafu kwa watumishi wa serikali<br>• Mfumo wa ajira na kupandisha vyeo kutegemea sifa<br>• Anzisha udhibiti wa uendeshaji<br>• Ugatuzi wa utaratibu wa kufanya maamuzi<br>• Hakikisha ufanyakazi wa mpango wa pensheni wa watumishi wa serikali. | • Kufuatilia uteuzi wa kazi wa serikali na kuripoti matendo ya rushwa<br>• Toshabikia shughuli za biashara na wala rushwa<br>• Fanikisha ubinafsishaji<br>• Fuatilia.kwa makini ubinafsishaji wa mashirika ya umma<br>• Saidia mazungu-mzo baina ya waajiri wa sekta binafsi na wa Serikali | • Kutia moyo watumishi wa serikali (1)<br>• Kuza ufanisi wa huduma za Serikali (2)<br>• Vutia wafanyakazi wenye vipaji kujiunga na utumishi wa serikali<br>Pandisha hadhi ya watumishi wa serikali |

| TATIZO | WIZARA (idara) | NANI ANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA TEKELEZWA AC=dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA LINI (13) Muda mfupi Des. 2000 (14) muda wa kati 2005 (15) muda mrefu: enye kuendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| | | | | | • Tathmini uwezo wa kiasasi na wa kiuongozi wa asasi za serikali kuu na serikali za mitaa<br>• Simamia ushikiliaji wa miko ya maadili<br>• Simamia ushikiliaji wa sheria, Kanuni, Taratibu na masharti ya Kudumu<br>• Toa mafunzo kwa wanafunzi wa kuchaguliwa kwa sifa waziwazi<br>• Boresha mazingira ya kufanyia kazi<br>• Pandisha kiwango cha uwezo wa asasi<br>• Boresha vifaa vya ofisi zana za mawasiliano n.k. | | |

| TATIZO | WIZARA (idara) | NANI ANUFAIKA | NANI ANAPOTEZA | MAMBO YALIYOKWISHA TEKELEZWA AC=dhidi ya rushwa | MAMBO YA KUTEKELEZWA | | MATOKEO YANAYOTARAJIWA NA LINI (13) Muda mfupi Des. 2000 (14) muda wa kati 2005 (15) muda mrefu: enye kuendelea |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Serikali | Raia | |
| | | | | | • Kazania asasi muhimu (Mahakama, Hospitali, Shule n.k.)<br>• Chukulia hatua kali za fundisho dhidi ya wafanyakazi wala rushwa. | | |